



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



RATIBA YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE
(STANDARD FOUR NATIONAL ASSESSMENT TIMETABLE)
OKTOBA, 2021

| TAREHE NA SIKU | MUDA (SAA) | NAMBA MFICHO | SOMO |
|--------------------------------------|--------------------|--------------|---|
| 28.10.2021 ALHAMISI | 2:00 – 3:30 | 01 | KISWAHILI |
| | 3:30 – 4:30 | | MAPUMZIKO |
| | 4:30 – 6:00 | 04 04E | HISABATI MATHEMATICS |
| | 6:00 – 8:00 | | MAPUMZIKO |
| | 8:00 – 9:30 | 05 05E | SAYANSI NA TEKNOLOJIA SCIENCE AND TECHNOLOGY |
| 29.10.2021 IJUMAA | 2:00 – 3:30 | 03 03E | MAARIFA YA JAMII SOCIAL STUDIES |
| | 3:30 – 4:30 | | MAPUMZIKO |
| | 4:30 – 6:00 | 02 | ENGLISH LANGUAGE |
| | 6:00 – 8:00 | | MAPUMZIKO |
| | 8:00 – 9:30 | 06 06E | URAIA NA MAADILI CIVIC AND MORAL EDUCATION |

MAELEKEZO MUHIMU

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Upimaji wa mwaka 2021** iliyoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
2. **Kabla ya kufungua bahasha** yoyote yenye maswali ya upimaji, hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kujihakikishia kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Upimaji**.
3. Endapo utata utajitokeza kati ya **maelekezo yaliyomo ndani ya Karatasi ya Upimaji na Ratiba ya Upimaji, maelekezo yaliyomo katika karatasi ya upimaji husika ndiyo yatakayofuatwa.**
4. Wanafunzi **WASIOONA** na wale wenye **UONI HAFIFU** waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa upimaji **wote** isipokuwa **DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa somo la **Hisabati**.
5. Msimamizi wa Wanafunzi **WASIOONA** awe mtaalamu mwaminifu aliye na **uwezo wa kusoma maandishi na alama za 'Braille'**.
6. Wanafunzi wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za upimaji na kujibia zenye **maandishi yaliyokuzwa** na zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.
7. Wanafunzi waelekezwe;
 - (a) Kuingia ndani ya chumba cha upimaji nusu saa kabla ya muda wa upimaji na watakaochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya upimaji kuanza hawataruhusiwa.
 - (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa upimaji.
 - (c) Kuandika jina kamili na namba ya upimaji kwa usahihi.
 - (d) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina yao. Ikiwa mwanafunzi ana tatizo anatakiwa kunyoosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa upimaji.
 - (e) Watakaojihusisha au watakaofanya udanganyifu watafutiwa matokeo yao ya upimaji.